VINTAGE EXAMS

DARASA LA NANE - 2018

SEHEMU YA KWANZA
KISWAHILI LUGHA.

Muda: Saa 1 Dakika 40

SOMA KWA MAKINI MAAGIZO YAFUATAYO.

1. Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibia. Kijitabu hiki kina maswali 50.
2. Ikiwa utataka kuandika chochote si jibu andika katika kijitabu hiki.
3. Ukisha chagua jibu lako lionyeshe katika **KARATASI YA MAJIBU** na wala sio katika kijitabu hiki cha maswali.

JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU.

4. Tumia penseli ya kawaida.
5. Hakikisha ya kwamba yafuatayo yameandikwa katika karatsi ya majibu.

NAMBARI YAKO YA MTIHANI
JINA LAKO
JINA LA SHULE SHULE YAKO

6. Kwa kuchora kistari katika visanduku vyenye namba zinazokuhusu, onyesha namba yako kamili ya mtihani (yaani namba ya shule, na zile namba tatu za mtahiniwa) katika sehemu iliyotengwa mwanzo wa karatasi ya majibu.
7. Usitie alama zozote nje ya visanduku.
8. Iweke safi karatasi yako ya majibu.
9. Kwa kila swali 1-50 umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi A, B,D na D. Ni jibu **MOJA** tu kati ya hayo manne ambalo ni sahihi. Chagua jibu hili.
10. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.

Mfano
Katika kijitabu cha maswali:
Kamilisha methali ifuatayo;
21. Asiyekujua
    A. hakudhamini
    B. hakuthamini
    C. hakutakii mema
    D. hakuambii toka

Jibu sahihi ni **B** (hakuthamini)
Katika karatasi ya majibu
20. [A] [B] [C] [D] **21.** [A] [~~B~~] [C] [D] **22.** [A] [B] [C] [D] **23.** [A] [B] [C] [D]

Katika visanduku vinavyoonesha majibu ya swali namba 21, kisanduku chenye herufi B ndicho kilichochorwa kistari.

11. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako kiwe cheusi na kisijitokeze nje ya kisanduku.
12. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku kimoja tu kati ya visanduku ulivyopewa.

Kitabu hiki cha maswali kina kurasa 7 zilizopigwa chapa

Geuza ukurasa

Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1-15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya vale uliyopewa.

Haki za mtoto ni ____1____ . ____2___ ya haki hizo ni elimu. Mtoto ___3____ budi ___4___ na shule punde tu ___5___ umri wa kwenda shuleni. Huko shuleni asome kwa bidii za___6___atengenezaye sega kwa nta. ____7____ hakufai kabisa shuleni. Yeyote anayezembea masomoni aelewe kuwa ____8____.

1.	A. maradufu	B. akili	C. anuwai	D. maridhia
2.	A. Kati	B. Katikati	C. Baadhi	D. Miongoni
3.	A. ana	B. yuko	C. alikuwa	D. hana
4.	A. kuungwa	B. kujisajili	C. kujiunga	D. kusajili
5.	A. afikapo	B. afikiapo	C. afikishapo	D. afikishavyo
6.	A. mchwa	B. mwanafunzi	C. nyuki	D. msomi
7.	A. kulaza damu	B. kutia fora	C. kukanyaga chechele	D. kufa kikondoo
8.	A. Elimu ni taa gizani huzagaa		B. Ajizi ni nyumba ya njaa	
	C. Bidii haiondoi kudura		D. Baada ya dhiki ni faraja	

Mkono wa Farida ___9___ na nyoka, ___10___ alipoelewa umuhimu wa afya; yaani ___11___. Alikonda kama ___12___ hadi akawa ___13___.Sumu ya nyoka ___14___ mwili wake sana. Namna siku ___15___ ndivyo alivyoendelea kukonda.

9.	A. alivyoumwa	B. ulivyoumwa	C. alipoumwa	D. ulipoiumwa
10.	A. ndipo	B. ndivyo	C. ndio	D. ndiye
11.	A. siha	B. siya	C. rahi	D. rayi
12.	A. sindano	B. ng'onda	C. mgonjwa	D. rayi
13.	A. gogo la mtu	B. nofu la mtu	C. pandikizi la mtu	D. gofu la mtu
14.	A.aliathiri	B. iliathiri	C. iliadhiri	D. iliadhiri
15.	A. zilisonga	B. zilivyoenda	C. zilivyosonga	D. zilienda

Kutoka swali 16 hadi 30, jibu kulingana na maagizo.

16. **Ki** katika sentensi . " Mwanafunzi huyo akikuona atatembea kijeshi" imetumiwa kuonyesha;
A. masharti, nomino
B. wakati, nomino
C. masharti, namna
D. wakati, namna

17. Tikiti, limau na fenesi ni mifano ya;
A. nafaka
B. mimea
C. matunda
D. mazao

18. Chagua [illegible] linaloonyesha kitenzi kilichoundwa [illegible] na kivumishi
A. Mzuri - [illegible]
B. Mcheshi - cheka
C. Mapishi - mpishi
D. Vumilia - mvumilivu

19. Chagua maelezo sahihi
A. Siku ya kwanza ya wiki ni jumatatu
B. Mtoto wa umbu nitamwita mokoi
C. Utosi ni sehemu ya mbele ya kichwa
D. Mtoto wa kwanza kuzaliwa huitwa chudere

20. Ni sentensi ipi iliyo na istiara?
A. Amina ni chiriku
B. Chakula hiki ni kitamu kama asali
C. Mlango ulimkondolea macho kwa dharau
D. Yeye ni mweusi tititi.

21. Kanusha;
Chakula kilichoiva kimeisha.
A. Chakula kilichoiva hakijaisha
B. Chakula kisichoiva hakujaisha
C. Chakuala kilichoiva hakikuisha
D. Chakula kisichoiva hakikuisha

22. Nje ni kweupe;
A. pepepe
B. kwekwekwe
C. papapa
D. kwikwikwi

23. Mfalme ni kwa malkia ilivyo mjomba ni kwa;
A. shangazi
B. ami
C. halati
D. amu

24. Karibu imetumikaje katika sentensi ifuatayo?
Mkirudi mjini, karibuni tena.
A. makaribisho
B. maagano
C. nusura
D. umbali

25. Tambua aina za maneno yaliyopigiwa vistari.
Vitabu vizuri vimewekwa vizuri
A. kielezi, kielezi
B kivumishi, kivumishi
C. kielezi, kivumishi
D. Kivumishi, kielezi

26. Tambua neno baki
A. lala unono
B. alamsiki
C. kwaheri
D. sabalheri

27. Iwapo kesho ni Jumamosi , juzi ilikuwa;
A. Jumapili
B. Alhamisi
C. Jumatano
D. Ijumaa

28. Ni sentensi ipi iliyotumia kiunganishi ifaavyo
A. Lau angalimsikiliza mama yake asingalitaabika
B. Musa ni mfupi bighairi ya nyumdo
C. Madhali ya hayo , tuanze safari
D. Sembuse umefika , chakula pesa zako

29. Ni methali ipi isiyofaa katika kundi hili?
A. Umoja ni nguvu utengano ni udhaifu
B. Mkataa wengi ni mchawi
C. Kifo cha wengi ni harusi
D. Kidole kimoja hakivunji chawa

30. Musa, Nairobi, Alhamisi na Desemsba , zote ni
A. nomino za pekee
B. nomino za jumla
C. nomino za wingi
D. nomino za kawaida.

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31-40.

Mtaa wa Ingusi katika gatuzi la Kakamega ulijulikana kote na takriban kila mmoja. Wakazi wa mtaa huo walikuwa na juhudi chungu nzima kazini. Aidha , wengi wao walikuwa mabwenyenye wenye heła si haba. Waliishi maisha ya umoja na mshikamano mkubwa. Daima dawamu, walifahamu kuwa umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu.

Mtaa huo ulikuwa na dosari moja. Ulikuwa mtaa wa wapendaanasa mno. Nyuma ya nyumba ya Mate, palikuwa na jumba la starehe ambalo lilikuwa maarufu kwa uuzaji wa vileo. Licha ya jitihada za utawala kujaribu kuwaasa raia kutojiingiza katika uraibu wa vileo , yote yalionekana yasiyowahusu ndwele wala sikio. Wale waliokwisha kuzama katika lindi na bahari ya anasa, katu hawakutaka kubanduka. Vikao vya wazi viliandaliwa ili kuwapa mwongozo wanakijiji lakini wapi! Waliyapuuza na kuwaona washauri kama watu wasio na lolote la maana ila kutaka kupata cha tumbo. Kwa jumla, wengi wa kijiji walikosa mwelekeo wakawa wasiombilika wala kusemezeka. washauri wakawaweka macho tu ili kusubiri yatakayotokea halafu. Walifahamu kuwa cha kuvunjika.....!

Katika jumba lile la starehe, palitokea dada fulani aliyewavutia watu sana. Alikuwa mrefu wa wastani ni pua ya kitara. Kinu chake cha nyigu na macho yake ya kusinzia viliwateka bakunja wote waliomwona. Alitokea kuwa mcheshi mno; jambo ambalo lilimpa uwezo wa kutangamana na wanakijiji kwa urahisi na wepesi mno. Kila mteja wa pale Rumbaraha alitaka kupata wakaa wa kusema naye faraghani. Binti mwenyewe alikwepa kulitumia jina lake halisi la Mava, akawa akipenda mno lakabu ya chombo.

Binti huyu alitumia vyema mlahaka wake ili kuiendeleza biashara yake ya siri. Alikuwa mwuzaji wa aina fulani ya asali ambayo ilikuwa tamu zaidi kwa mwenye kuilamba. umaarufu wake na bidhaa hii ulidhihirika pale ambapo wateja wake wa kiume waliamua kuonyesha umahiri wao. Walishikana na kuanza kupigana kwa madai ya kuingilia uhusiano wao.

Kila mmoja alidaia kuwa ndiye aliyefahamiana tosha na yule dada. Kukuru kakara zile ziliendelea kwa muda wa saa nzima hadi pale ilipowabidi walinda usalama kuwafukuza wote wawili. Mwanadada alionekana mwenye furaha akawa anatabasamu kuashiria ushindi. Mwenzake alipomkumbusha yaliyotokea aliangua kicheko kama fisi na kudai kuwa "Nimewarambisha sumu tamu hadi wakajisahau. Potelea mbali, wajinga ndio wali wao. "Aliyeambiwa haya aliyaweka moyoni akawa anawaza na kuwazua kilichoitwa sumu tamu.

31. Mtaa huo ulikuwa na dosari moja yaani ulikuwa na;
A. kasoro moja
B. faida moja
C. jambo moja
D. ushindi mmoja

32. Yalionekana yasiyowahusu ndwele wala sikio ndiko kusema kuwa;
A. waliyaona ni upuuzi
B. waliyachukua na kuwapuunza
C. waliyachukulia kuwa ya upuuzi
D. waliyashika yakawa ya upuuzi

33. Walipopewa ushauri , waliowaona waliowapa ushauri kama watu ovyo
A. waliotaka la kuji ufaisha tu
B. waliokosa pa kujifanishia
C. waliyachukulia kuwa ya upuuzi
D. waliyashika yakawa ya upuuzi

34. Baada ya juhudi na jitahada zao kugonga mwamba washauri walielewa kuwa cha kuvunjika;
A. huliliwa kweli
B. hupelekekwa fundi
C. halina fundi
D. hakina rubani

35. Maneno viliwataka bakunja yana maana kuwa
A. viliwapumbaza
B. viliwazindua
C viliwazingua
D. viliwaangamiza

36. Kilichomfanya Chambo kutangamana na wananchi kwa urahisi mno ni;
A. ghiliba zake
B. biashara zake
C. tamaa ya wanaume
D. ucheshi wake

37. Kwa kurejea aya ya pili, chambo alikuwa
A. mrembo wa tabia
B. mrembo wa maneno
C. mrembo wa sura
D. mrembo wa maumbile

38. Mbali na vileo vilivyouzwa pale Rumbaraha,
A. Chambo aliuza sumu haramu
B. Chambo aliuza sumu tamu
C. Chambo aliwauzia wanaume pombe kali
D. Chambo aliwateka bakunja wanaume wa Rumbaraha.

39. Yamkini wanaume waliopigana walikuwa na nia ya
A. kujitolea kwa kumlinda chambo
B. kuonyesha imani yao kwa Chambo
C. Kuonyesha utajiri wao kwa Chambo
D. Kuonyesha mapenzi yao kwa Chambo

40. Chambo alisema kuwa "Nimewarambisha sumu tamu" unadhani alimaanisha nini?
A. Alikuwa amewaambukiza Ukimwi
B. Alikuwa amewagawia ukimwi
C. Alikuwa amewapa sumu ambayo ni tamu kutamba
D. Aliwapa asali iliyihariniwa chupani.

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali. 41- 50.

Maliasili katika nchi yetu yana faida chungu nzima. Taifa letu limepiga hatua kubwa kiuchumi kwa sababu ya kutegemea maliasili. Tuna mifano mingi mno ya maliasili. Mathalani, wanyamapori, maji na mito , madini, milima na vilima, miti na kadhalika. Serikali imejitolea mhanga kuwahamisisha wananchi kuhusu maliasili na umuhimu wake. Siku moja nilihudhuria mkutano ulioandaliwa na serikali ili kusikiliza hotuba iliyohusu mojawapo ya maliasili.

Baada ya kila mtu kutulia tuli, mfawidhi alianza, "Mgeni mheshimiwa , wageni walikuwa, mabibi kwa mabwana, nachukua fursa hii adimu na adhimu kusimama mbele yenu na kusema machache japo ya muhimu kuhusu miti. Awali ya yote, ninachukua fursa hii kumshukuru Raufu kwa kutujaalia siku hii angavu na tulivu.

Mti ni moja kati ya mimea yenye manufaa belele kwetu. Kwa kuegemea manufaa au faida tunazopata kutokana na mti, nina haki ya kudai kuwa mti ni uhai. Kwanza, miti hutupa vyakula kwa njia ya matunda. Tunapoyala, afya zetu huweza kuimarika nasi tukaweza kufanya kazi ipasavyo. Pili, miti huunda misitu na kwa njia hiyo huweza kuvutia mvua licha ya kurembesha mazingira. Miti ni pambo la nchi.

Nchi yetu hutegemea pakubwa pesa za kigeni. Wageni aghalabu huja kuzuru nchi yetu ili kujionea wanyama aina mbalimbali kama vile ndovu, chui, twiga, nyati na hata viboko. Ni kweli kuwa wanyama hawa huishi msituni . Hatubishi! Miti ni makao ya wanyama

Zipo baadhi ya nyumba ambazo hujengwa kwa kutumia miti. Ndani. nyumba hizi huwa na fanicha. yaani vyombo ambavyo hutokana na miti. Tusisahau kuwa baadhi ya miti dawa ambazo hutusaidi kudhibiti maradhi mbalimbali kuna vitabu ambavyo sisi hufurahia kuvisoma. Karatasi zinazounda vitabu hivyo hutoka kwenye miti. Maeneo yenye miti yana rotuba kwa kuwa mbali na miti kushikilia udongo, majani yake huweza kufanya mboji udongoni.

Tunastahili kutunza miti kwa udi na uvumba kwani ni dhahiri shahiri kuwa miti ikikosekana nchi yetu itaangamia. Wanaoharibu miti kwa kuchoma makaa ama kupata maeneo ya kukaa au kulima wachukuliwe hatua kali ili liwe funzo kwao na wenye nia kama hiyo. Tukitoka hapa ninawasihi nyote kutafuta angalau miche miwili na kuipanda halafu muitunze hadi kukua kwake. Hadi tutakapokutana tena, ninawashukuru kwa kunisikiliza na kuitetea miti. Mola awe nanyi. Asante na kwaheri ya kuonana."

41. Anayehutubia anayatumia maneno "fursa hii adimu" na adhimu kumaanisha kuwa
A. si nadra wal muhimu
B. si nadra ila muhimu
C. hatakuwa nadra ingawa muhimu
D. ilikuwa nadra na muhimu

42. Neno **Raufu** lilivyotumika bila ya shaka ni;
A. jina la Mungu
B. sifa ya Mungu
C. kurejelea Mungu
D. kumtija Mungu

43. Msemaji anadai kuwa ana haki ya kusema kuwa miti ni uhai kutokana na
A. manufaa kiduchu ya miti
B. faida tele za miti
C. manufaa machache ya miti
D. bei tahafifu ya miti

44. Kwa maoni ya msemaji, miti huchangia vipi uimarishaji wa afya zetu;
A. kwa kutupa vyakula vya kujenga mwili
B. kwa kutupa vyakula vya kulinda mwili
C. kwa kutupa vyakula tukijenga mwili
D. kwa kutupa vyakula vya kukinga mwili

45. Kulingana na maelezo katika aya ya tatu
A. miti ni pambo la nchi
B. miti ni pambo la misitu
C. miti ni pambo la shule
D. miti ni pambo la mazingira

46. Watalii wajao nchini kwa wingi huvutiwa mno na wanyama waishio msituni
A. hivyo miti hiuhifadhi wanyama
B. kwa kaunti hii miti ni makao ya wanyama
C. kw misingi hii miti huwavutia wanyama
D. kwa maana hiyo miti hukuza wanyama

47. Miti hutupa mbao nyingi;
A. ambazo huunda fanicha
B. hutumika huundisha fanicha
C. ambazo hutumika kuunda samani
D. hutumika kuundana samani

48. Msemaji anatyoa matumizi mangapi ya miti?
A. Thenashara
B. Manane
C. Matano
D. Edashara

49. Msemaji anamaanisha nini anaposema, "kwa udi na uvumba"?
A. kwa hali na mali
B kwa namna yoyote
C. kwa jino na ukucha
D. kw pupa na papara

50. Kifungu hiki kinahusu ;
A. umuhimu wa mazingara
B. umuhimu wa mazingira
C. umuhimu wa maliasili
D. umuhimu wa miti